

# KISWAHILI

MUDA: SAA1 DAKIKA40

Kifungu kifuatacho kina nafasi 1-15. Jaza kila nafasi ukitumia jibu sahihi kutoka kwa yale uliyopewa.

Kuku 1 mayai 2 sana. Mayai hayo yalikuwa kwenye choto kisha 3 kwa muda wa 4 matatu hivi kisha 5 vifaranga 6 walikuwa na rangi tofauti kuku alilinda vifaranga 7 wasiliwe na 8.

Siku 9 kuku aliwatisha vifaranga kwenye mbawa 10. Mwewe naye alifanya ujanja na kuangusha punje 11 mahindi karibu. Kuku 12 na kuangukia kwenye mlo wake. Kuku huyu 13 mahindi kwa furaha bila kufahamu ujanja wa mwewe. Mwewe aliwavamia vifaranga na kumchukua 14. Kuku alimlilia kifaranga wake lakini kilio si 15.

A	B	C	D
1. alizaa	aliangua	alitaga	aliteka
2. mengi	mingi	wengi	mwingi
3. akayalalia	akayaatamia	akayaramia	akayakalia
4. wiki	juma	miezi	majuma
5. yakaanguliwa	yakaliwa	yakaramia	akayalia
6. ambavyo	ambayo	ambaye	ambao
7. wake	vyake	vyao	zao
8. jogoo	mbuni	mwewe	njiwa
9. mmoja	kimoja	moja	mocha
10. yake	zake	yao	lao
11. la	ya	za	wao
12. alipuruka	alianguka	alidandia	alizama
13. alitafuna	alikekela	aliyadona	aliyagegeda
14. kimoja	mmoja	moja	wamoja
15. kizuri	dawa	tatizo	kibaya

**Kutoka swali la 16 - 30, jibu kulingana na maagizo.**

16. Neno kiwavi liko katika ngeli gani?  
 A. LI -YA                    B. U -U  
 C. KI -VI                    D. A - WA
17. Jibu la salamu, Buriani ni?  
 A. Binuru                    B. Chewa  
 C. Buheri wa afya        D. Buriani dawa
18. Tumia kiulizi - pi vilivyo.  
 Dawa \_\_\_\_\_ zilinunuliwa?  
 A. zipi                      B. yupi  
 C. ipi                        D. lipi
19. Siku ya Ijumaa huja \_\_\_\_\_ ile ya Alhamisi.  
 A. kabla ya                B. baada ya  
 C. na                        D. katikati ya
20. Andika sentensi kwa wingi.  
 Dawa hii ni chungu.  
 A. Dawa hii si chungu  
 B. Dawa hizi ni chungu.  
 C. Madawa hizi ni chungu.  
 D. Madawa haya ni machungu.
21. Tegua kitendawili  
 Kam̄ba yangu ndefu na haikunjiki?  
 A. Mshipi                    B. Kamba  
 C. Barabara                D. Uzi
22. Tumia amba kwa usahihi  
 Mazingira \_\_\_\_\_ ni safi hupendeza.  
 A. ambayo                    B. ambazo  
 C. ambao                    D. ambaye
23. Kamilisha methali ifuatayo.  
 Kamba ya mbali haifungi.  
 A. kuku                      B. nyoka  
 C. mwizi                    D. kuni
24. Tumia kiashiria kifaacho kwenye senten  
 Manyani \_\_\_\_\_ wameharibu mimea ye  
 A. wale                     B. zile  
 C. hizo                     D. yale
25. Ni neno lipi halifai kuwa kwenye orod  
 ifuatayo.  
 A. wodi                    B. machela  
 C. siriji                    D. ungo
26. Tumia nafsi sahihi  
 \_\_\_\_\_ anacheka sana.  
 A. Mimi                    B. Yeye  
 C. Wewe                    D. Nyinyi
27. Kanusha sentensi.  
 Mgeni amewasili.  
 A. Wageni wamewasili.  
 B. Mgeni hajawasili.  
 C. Mgeni hakuwasili.  
 D. Mgeni hatawasili.
28. Sehemu iliyotiwa rangi ni  

- A. tusui tatu                B. subui  
 C. subui tatu                D. tatu subui
29. Chagua kielezi kwenye sentensi.  
 Nyumba yako imepakwa rangi.  
 A. rangi                    B. nyumba  
 C. yako                    D. imepakwa
30. Vazi gani kati ya haya huvaliwa na wanawaka  
 kushikilia maziwa.  
 A. chupi                    B. gaguro  
 C. gauni                    D. kanchiri

Soma kifungu kifuatacho kisha uiibu maswali 31-40

Ngombe ni mnyama mojawapo anayefungwa na binadamu. Ni mnyama mkubwa sana anayefanana na nyati. Chakula chake kikuu ni nyasi.

Ng'ombe ana miguu minne ambayo ina makanyagio magumu yaitwayo kwato. Vilevile ana pembe mbili ambazo hutumia hasa kuwagolea maadui zake. Licha ya hayo, ana mkia mrefu unaotumika kuwafukuza nzi na wadudu wengine.

Mnyama huu ana faida nyingi mno. Nyama nyingi inayoliwa na binadamu ni ya ng'ombe. Nyama ya ng'ombe ndiyo huliwa sana kwa sababu si ghali sana ukilinganisha na kuku, nguruwe, mbuzi na kondoo. Nyama hii huliwa kwa kuchemshwa au kuchomwa na kukifanya kitoweo kuwa kitamu kupindukia.

Licha ya hayo ng'ombe hutufaidi kwa ngozi yake. Ngozi hizi nazo hutumika kutengeneza vitu vingi kama vile viatu, mishipi, mikoba na kadhalika. Ngozi pia ilitumika kizamani hata sasa kutengeneza silahi kama nqao ambazo zilitumika kuiikinga wakati wa vita.

Nayo maziwa tunayokunywa hutoka wapi? Pengine ng'ombe wengi hufungwa kwa minajili ya kutupa maziwa. Maziwa ni chakula muhimu sio tu kwa watoto wachanga bali kwa watu wote. Maziwa hunywewa moja kwa moja, hutumika kupikia chai, hutiwa katika mboga zinapopikwa na mengi mengineyo.

Vilevile kwato za ng'ombe hutumika kutengeneza gundi. Gundi nayo hutumika kufanya kazi nyingi hasa ofisini. Ama kweli, ng'ombe wana umuhimu sana

31. Kulingana na ufhamu  
A. ng'ombe hufanana na kondoo.  
B. ng'ombe hufanana na mbuzi.  
C. ng'ombe hufanana na nyati.  
D. ng'ombe hufanana na pundamilia.

32. Chakula anachokula ng'ombe ni  
A. nyasi  
B. nyama  
C. maziwa  
D. mchanga

33. Makanyagio ya ng'ombe huitwa  
A. fumba                    B. nyayo  
C. kwato                   D. kwata

34. Sehemu hizi ni za ng'ombe ila  
A. mkia mrefu            B. kwato  
C. pembe                   D. mkonga

35. Kutokana na ufhamu ni sawa kusema  
A. ng'ombe hutaga mayai.  
B. nyama.  
C. nyama ya ng'ombe huliwa sana.  
D. nyama ya kuku huliwa sana kuliko kuku.

36. Ng'ombe hutumia pembe zake kivipi?  
A. Kuwavutia wenzake.  
B. Kugotea maadui.  
C. Kukimbilia.  
D. Kulia nyasi.

37. Ngao ni zana ya vita inayotumika  
A. kumshambulia na kumdunga adui.  
B. kujikinga dhidi ya adui.  
C. kumkata adui.  
D. kumwangia adui.

38. Maziwa hunywewa na  
A. maajuzu                B. mashaibu  
C. watoto                   D. kila mtu

39. Kwato za ng'ombe  
A. hutupwa.  
B. huliwa.  
C. hutumika kutengeneza gundi.  
D. hutupa maziwa.

40. Kichwa kifaacho taarifa hii ni  
A. Faida za ng'ombe.  
B. Hasara za ng'ombe.  
C. Maziwa na ng'ombe.  
D. Nyama.

**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 41-50.**

Lilikuwa jambo la kushangaza liliwafanya waombalezaji kutimua mbio kwa woga baada ya kijana aliyekufa kujitokeza wakati wa matanga yake. Maajabu haya yalitokea uswahilini wakati wa adhuhuri "Mzimu" wa Elisha Muge alionekana akiwasalimia watu bila kuzungumza. Watu walianza kutoroka. Akina baba na babu wahama "miguu tuponye" Mzimu huyo alipelekwa kwa mganga aliyeogopwa kwa ujuzi wake wa kuchunguza mambo kama hayo.

Mwosha alikolazwa Elisha naye aliitwa kuitambua sura ile matata ya mzimu yule. Baada ya mwosha kumkagua kwa makini, alisema wazi kuwa alikuwa ni Elisha aliylazwa katika mochari.

Watu wengine walionyesha ujasiri wa kukaa pale walijaribu kumzungumzia Elisha lakini hakuzungumza alitiikia tu kwa mabega yake.

Muda si muda, mama yake marehemu na waombalezaji wengine walichomoka kutoka kwenye kibanda na kuanza kumsifu Mungu aliyewafufulia mtoto wao. Waandishi wa habari walifika kujionea maajabu yale! Ama kweli, dunia ina mambo!

- |  |  |
|--|--|
| 41. Ni jambo gani liliowashangaza waombalezaji?<br>A. kuzaliwa tena kwa Elisha.<br>B. Kutimua mbio kwaz watu.<br>C. Kufufuka tena kwa Elisha.<br>D. Kuja kwa mganga na mwosha. | 46. Wa mwisho kufika katika eneo lile la kuomboleza alikuwa?<br>A. akina bibi na babu.<br>B. waganga.<br>C. wanahabari.<br>D. hatujui. |
| 42. Mzimu wa Elisha alionekana<br>A. akiwasalimia watu.<br>B. akichekesha watu.<br>C. akikimbia.<br>D. akizungumza kwa sauti.  | 47. Mkasa huu ulitokea wapi<br>A. mochari<br>B. usiku<br>C. jioni<br>D. mchana   |
| 43. Kwa maoni yake mwosha ni<br>A. mtu anayeosha maiti.<br>B. mtu anayeishi na maiti.<br>C. mtu alaye na maiti.<br>D. mtu alaye maiti.   | 48. Unadhani, maajabu haya yalitokea saa ngapi?<br>A. asubuhi<br>B. usiku<br>C. jioni<br>D. mchana                                     |
| 44. Mtui aliyekufa huifadhiwa<br>A. kaburini<br>B. mbinguni<br>C. sandukuni<br>D. mocharini  | 49. Maana ya miguu niponye ni<br>A. kuumia miguu.<br>B. kukimbia.<br>C. kuvalia viatu.<br>D. kutibiwa miguu.                           |
| 45. Jina la heshima kwa aliyekufa ni<br>A. shetani<br>B. malaika<br>C. hayati<br>D. mzee   | 50. Kichwa mwafaka cha taarifa hii ni?<br>A. Mtu afufuka.<br>B. Mgonjwa hospitalini.<br>C. Maajabu ya waganga<br>D. Mkasa wenye raha.  |